# Kituo cha Kushughulikia Majanga cha Waterbury Kitafungwa Tarehe 12 Okoba

**Release Date: Oktoba 11, 2024**

Kwa uratibu wa jimbo na washirika wa ndani, tutafunga kabisa Kituo cha Kushughulikia Majanga (DRC) cha Waterbury saa 6 p.m. Jumapili, tarehe 12 Oktoba, 2024.

Kituo hiki kwa sasa hufunguliwa saa 9 a.m. hadi saa 6 p.m. Jumatatu hadi Jumamosi:

- Waterbury Armory - 294 Armory Drive, Waterbury, VT 05676

**Kama mbadala**, Wakazi wa Vermont wanaweza kutembelea vituo (DRCs) vingine viwili kwa sasa vinafunguliwa saa 9 a.m. hadi saa 6 p.m. Jumatatu hadi Jumamosi:

- Lyndonville Public Safety Facility - 316 Main Street, Lyndon, VT 05851
- Hinesburg Town Hall - 10632 Route 116, Hinesburg, VT 05461

Kufungwa kwa vituo hivi vya muda kumeratibiwa na jimbo na washirika wa ndani kulingana na idadi ya wanaotembelea na mahitaji ya jamii.

## Siku ya Mapumziko ya Kitaifa

Vituo vya Kushughulikia Majanga vya Vermont vitafungwa Jumatatu, tarehe 14 Oktoba ili kuadhimisha Siku ya Wazawa na Siku ya Columbus. Vitafunguliwa tena **Jumanne, tarehe 15 Oktoba** saa za kawaida.

Wakazi wa Vermont walioathiriwa na dhoruba zote mbili za Julai wanaweza kutembelea Kituo cha Kushughlikia Majanga ili kupata msaada wa ana kwa ana kutoka FEMA na Utawala wa Biashara Ndogo wa Marekani. Kwa taarifa za hivi punde kuhusu sehemu na saa, tembelea fema.gov/drc.

Pia kuna **njia zingine tatu** za kuomba ambazo hazihitaji kutembelea kituo:

- Nenda mtandaoni kwa DisasterAssistance.gov.
- Piga Simu ya Usaidizi ya FEMA kwa **800-621-3362**.
- Pakua Programu ya Simu ya FEMA.